TANGAZO LA SERIKALI NA. 877 la tarehe 1/12/2023

SHERIA YA USIMAMIZI NA TOZO YA USHURU,
(SURA YA147)

---

# AMRI

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

## AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MAWILI YANAYOINGIZWA NCHINI NA WAWAKILŸ`ΩISHI WA SHIRIKA LA WAKIMBIZI DUNIANI NCHINI TANZANIA YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Mawili Yanayoingizwa Nchini na Shirika la Wakimbizi Duniani nchini Tanzania ya mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 3 Novemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachopaswa kulipwa kuhusiana na magari mawili yaliyoainishwa katika Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha kwaniaba ya Shirika la Wakimbizi Duniani kwa ajili ya shughuli za UNHCR-Kasulu umesamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 01 Mei, 2024

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| SN | Maelezo | Namba ya Injini | Idadi | Namba ya Chassis | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Coster Bus W/cooler, 29 seats, high roof, 4.2 diesel, model HZB70R – ZGMSS-P1 | 1HZ-1055797 | 01 | JTGABCB8406720386 | Imeingizwa |
| 2 | Toyota Coster Bus W/cooler, 29 seats, high roof, 4.2 diesel, model HZB70R – ZGMSS-P1 | 1HZ-1054622 | 01 | JTGABCB8106720376 | Imeingizwa |

Dodoma,
21 Novemba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*